# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL5

# KISWAHILI PAPER 3 ANSWERS

**SEHEMU YA A (Alama 20 )**

**USHAIRI**

**1. (a) Mama. Kinda ninakulilia. (kichwa chochote mwafaka alama 2)**

**(b) Huzuni. Kilio.**

**(c) Tunu za dunia/raha.**

**Urembo wa shani. N**

**goma/kucheza ngoma.**

**(d) Jazanda-kinda mtini.**

**Tashhisi –sauti uliyotoa imenigusa moyoni**

**Tabaini-si mbwa wala si nyani.**

**Tashtiti/balagha- ubeti wa 9 mshororo wa 3. (zozote 2x2=alama 4)**

**(e) Uhuru.**

**(i) Inkisari/ufupisho/makato. k.m kimojapo-kimojawapo.**

**(ii) Kuboronga sarufi –kinda ninakulilia-ninakulilia kinda.**

**(iii) Mazida –kuikumbukia-kuikumbuka. (hoja moja 1x2=alama 2)**

**(g) (i) ghuma –mshangao/huzuni.**

**(ii) sumbuku- mkiwa.**

**SEHEMU YA B (Alama 20 )**

**RIWAYA**

**2. 2(a)**

**-Msemaji ni Bi Zuhura.**

**-Anajiambia mwenyewe.**

**-Yuko katika jumba lake akiwa pweke.**

**-Alikuwa akiwachwa na muwewe bila kumpa mapenzi. (alama 4)**

**(b)**

**-Mvumilivu- anavumilia tabia ya Bwana Nasaba Bora,na hata anyimwapo penzi,hajakuwa na jicho la nje.**

**-Ana utu –anamhurumia Uhuru na anamsadia licha ya kuwa na walakini kuwa mtoto wa mumewe,Anataka DJ ashughulikiwe baada ya kuumwa na Jimmy.**

**-Mlezi mzuri –Licha ya Mashaka kuwa kama wazimu;anamshughulikia.Pia malezi yake kwa madhubuti yanamfanya anakuwa na msimamo mzuri kuhusu maisha.**

**-Msamehevu-hata baada ya kutalikiwa anahudhuria mazishi ya mumewe.**

**-Mwenye huruma-Anamrai mumewe awaachilie Amani na Imani kutoka gerezani,vile vile anamtaka mumewe amsadie yule mama mjamzito na hata kumbeba Amani.(zozote 2x2=4)**

**(c) Jazanda –ndoa kulinganishwa kuwa kama mashua ambayo ina abiria wengi: waume na wake.**

**-Taswira-picha ya abiria wakiabiri mashua (ndoa) (zozote 2x2=4)**

**(d) -Wanawachia malezi ya watoto-k.m Mwalimu Majisifu hasaidii Dora kuwatunza wanao: lake ni ulevi tu.**

**-Wananyimwa mapenzi- Dora ananyimwa mapenzi kwa miaka 15 na Bi Zuhura vile vile ananyimwa haki ya ndoa.**

**-Wanaume hawawezi kuwasaidia hata wanawake wajawazito ilivyokuwa kwa mama aliyekuwa akijifungua na Mtemi hakumsaidia.**

**-Wanawake wengine hawana maamuzi yote yanafanywa na wanaume k.m Lowela anamwacha mawanaye kwa Amani kwani aliambiwa na Mtemi.**

**-Wanawake wananyang'anywa mali yao;hawana usemi mbele ya baadhi ya wanaume k.m mamake Imani aliyenyang'anywa shamaba na Nasaba Bora.**

**-Wanashurutishwa kuhudhuria mikutano ya hadhara k.m Bi.Kizee: wangetumia muda huo kujiendeleza kimaisha kwani hata hawaelewi kisemwacho.**

**-Wanafungwa jela bila kujali jinsia yao k.m Imani anafungwa jela pamoja na Amani na Matuko Weye.(kutaja alama 1,maelezo alama 1)**

**(Hoja zozote 4x2=8)**

**3)**

**-Viongozi peke yao wanaonufaika na uhuru k.m kukuza mazao yaletayo faida Sokomoko baada ya wakoloni.**

**-Raia walitarajia kurejeshewa ardhi iliyotwaliwa na wakoloni lakini viongozi wananyakua ardhi hiyo k.m Nasaba Bora kunyakua mashamba ya Chirchir Hamadi na Mwinyi Hatabu Mtembezi.**

**-Viongozi wanaendeleza ufisadi unaowanyima raia matunda ya uduru,Mtemi Nasaba Bora alipokuwa katika Wizara ya Ardhi na Makao anajitengenezea faili za kupata mashamaba na pia kula mlungula.**

**-Serikali inawanyima raia matunda ya uhuru kwa kutumia misaada ya kupunguza umaskini kuwasomesha watu wasiostahimili k.m Fao ng'ambo. -Wengi wa Wanatomoko hawapati kufaidika matunda ya uhuru kwani hawapati huduma za afya k.m DJ na Uhuru.**

**-Mashujaa waliopigania uhuru wa Sokomoko wanatelekezwa badala ya kula matunda ya uhuru wa k.m Mzee Duni na Mzee Matuko Weye ambao wanaishi maisha duni.**

**-Wanatomoko walipigania uhuru lakini hawana uhuru wa kusema au kotoa maoni k.m Matuko Weye anatishwa na kutiwa mbaroni anapotoa usemi wa kukashifu uongozi.**

**-Wanatomoko wameridhia lugha ya wakoloni (kiingereza) badala ya kukuza lugha yao.Hata hotuba ya Mtemi inatolewa kwa kiingereza licha ya raia kutoilewa.**

**-Raia hawana uhuru wa kujiamulia,wakati wa sherehe za kuadhimisha siku kuu ya wazalendo,raia wanatiwa hofu,na kulazimishwa kuhudhuria sherehe.**

**-Wanatomoko wanaridhi elimu ya wazungu,wakoloni badala ya kujenga elimu yao k.m Nasaba Bora (Majisifu), Fao na Madhubutu –hawa wanaenda kusoma ng'ambo.**

**-Viongozi pekee ndio wanaoishi kwa makaazi bora k.m Nasaba Bora.**

**-Raia wengi hawana kazi wala mashamba.Ni baada ya uhuru wa pili ndipo Amani na Madhubuti wanawagawia mashamba.**

**-Serikali mpya inaendeleza ukatili-mamake Imani anapigwa na kufurushwa kutoka nyumba yake na shamba lake pia Chirchir Hamadi anauwawa.**

**SEHEMU YA C (Alama 20 )**

**TAMTHILIA**

**3. 4. (a)**

**(i) Yalisemwa na Mstahiki Meya.**

**(ii) Akajiambia mwenyewe.**

**(iii) Akiwa Ofisini mwake.**

**(iv)Alisema haya akirejelea mwanakandarasi ambaye atamfuta kazi (alama 4)**

**(b) Takriri (uradidi) kwa mfano safi,safi. Uzungumzi nafsi k.m safi,safi huyu nitamfurusha. (alama zozote 2x2=alama**

**4) (c) (i) Unafiki.**

**-Meya anajifanya anafanya kazi kwa manufaa ya umma ilhali anajinufaisha na washiriki wake k.m anajilimbikizia vipande vya ardhi.Pia anashirikiana na mwanakandarasi.**

**-Meya anajifanya mcha Mungu,mpole,mnyenyekevu na kwamba ana wito wa kumtumikia Mungu,jambo ambalo si kweli.**

**-Meya na baraza lake wanataka kuonekana wawajibikaji kwa mameya wan je ilhali si wawajibikaji.(zozote 3x1=alama 3)**

**Propaganda**

**-Meya alisema kuwa dawa zipo bandarini lakini hazipo.**

**-Kusema kwamba mji wa Cheneo ni wa kupigiwa mfano kimaendeleo ilhali si kweli.**

**-Anaposema kuwa wanachochewa na daktari Siki, jambo ambalo si kweli.(zozote 3x1=alama 3)**

**Ubadhirifu wa mali**

**-Meya anawapeleka watoto wake ng'ambo kusoma kutumia pesa za umma.**

**-Anapeleka mkewe kujifungua ng'ambo.**

**-Anampeleka mkewe kutibiwa mafua ng'ambo.**

**-Anapeleka Bili katika hoteli za kifahari.**

**-Kuwapa mameya (wafadhili) mapokezi katika hoteli ya kifahari na pia vyakula kutoka kila utamaduni duniani.**

**-Mvinyo kuagizwa kutoka urusi na Divai kutoka Ufaransa.**

**-Anawauliza madiwani kama anaweza kukarimu chochote wao wanaomba posho.**

**-Meya alimlipa mhubiri laki moja. (zozote 3x1=alama 3)**

**Usaliti**

**-Aliwasaliti wafanyakazi kwa kutowaongeza mshahara.**

**-Alimsaliti Diwani III kwa kutomshirikisha katika mkutano wa madiwani.**

**-Aliwasaliti wananchi kwa kuwanyang'anya viwanja na vipande vya ardhi na kuviuza.**

**-Aliwasaliti Wanacheneo kutowapatia elimu bora ilhali watoto wake wanasoma ng'ambo.**

**-Aliwasaliti wananchi kutohakikisha kuwa kuna chakula bora cha kutosha.**

**-Aliwasaliti wanacheneo kutobuni nafasi za kazi. (zozote 3x1=alalma3)**

**5. )**

**1. Ufisadi umekiti mizizi- mwanakandarasi.**

**2. Umaskini –wananchi wa kawaida kukosa chakula na hela za matibabu.**

**3. Uongo wa viongozi- kudanganya kwamba dawa zimeagizwa.**

**4. Ukoloni mamboleo – viongozi kuiga tabia na mienendo ya wakoloni k.m mvinyo ghali,kutembelea hoteli za kifahari.**

**5. Utegemezi wa misaada.**

**6. Vitisho k.m kutishia kuwavurumisha kazini wale wanaogoma.**

**7. Ukaragosi- kutotaka kupinga viongozi kwa ajili ya kujinufaisha kibinafsi.**

**8. Propaganda.**

**9. Kutumia vibaya vyombo vya dola k.m matangazo,askari kutumiwa kuwatawanya wanaogoma.**

**10. Viongozi kutowajibika k.m kutojali kifo cha mtoto kutokana na ukosefu wa matibabu.**

**11. Mishahara duni kwa wafanyakazi wa umma.**

**12. Ubadhilifu –kutumia pesa za umma kuingizia vinywaji ghali,kujistarehesha katika hoteli kubwa kubwa.**

**13. Unafiki wa kidini-viongozi kudai ni wacha Mungu ilhali wanawadhulumu raia,kuwapa mapdre pesa ili wapate uungwaji mkono.**

**14. Ushauri mbaya –Bili kushauri waibe na kuuza fimbo ya Meya.**

**15. Ujinga wa raia-kuendelea kuchagua viongozi wasiostahili mara kwa mara.**

**16. Mapinduzi –kutumia mbinu hasi kuondoa viongozi mamlakani hali inapoendelea kutoridhisha.**

**17. Kujiuzulu kwa wafanyakazi badala ya kuendelea kupigania mabadiliko.**

**18. Mazingira chafu –maji kukosekana kwenye makao ya akina yaha.**

**19. Uundaji wa kamati zisizokuwa na manufaa. Tanbihi –maelezo ni lazima,mwanafunzi arejelee tamthilia.**

**SEHEMU YA D (Alama 20 )**

**DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE:**

**4. 6.) a. Msemaji ni Fikirini.**

**o Anamwambia Fiona.**

**o Wako barabarani.**

**o Hii ni baada ya Fikirini kunaswa na polisi kwa kutofunga zipu na kutozwa faini ya dola mia mbili.**

**(4x1=alam**

**4) b. Fiona.**

**o Mwanamke mweusi pandikizi la miraba mine.**

**o Katili. o Mwongo.**

o Mwenye vitisho.

o Hajithamini.

o Mwizi.

o Mnafiki.

o Binafsi. (zozote 6x1=alama

6) c.

o Watu weusi wanabaguliwa katika nchi ya watu weupe.

o Wanaadhibiwa vikali kwa makosa madogo kwa kuwa weusi.

o Wahadhiri chuoni wanawapendelea wazungu.

o Walinzi kwenye maduka makubwa huwakagua zaidi.

o Dereva anampita Fikirini kwa kuwa ni mweusi.

o Wanafunzi wanakejeli Fikirini.

o Wanabaguliwa na weusi wa marekani kwa kuibiwa na kutishwa. (zozote 6x1=alama 5)

7.UONGOZI WA KIJAMII

o Uasherati/uzinzi samaki wan ci za joto,damu nyeusi,kanda la usufu.

o Ulevi na anasa-macko,mwana wa darubini,gilasi ya mwisho makaburini.

o Ubaguzi-maskini babu yangu,damu nyeusi.

o Kutoajibika- kikaza,mzizi na matawi, samaki wa nchi za joto.

o Tamaa- ndoa ya samani,tazamana na mauti..

o Uzembe –mke wangu. o Uavyaji mimba –samaki wa nchi za joto.

o Ujambazi –gilasi ya mwisho makaburini Damu Nyeusi.

o Biashara haramu –Samaki wa nchi za joto.

o Ukabila –maskini babu yangu.

o Ubakaji-mwana wa darubini.

o Ubinafsi- ndoa ya samani,tazamana na mauti,mwana wa darubini.

**o Uongo – mzizi na matawi,kikaza,mwana wa darubini.**

**SEHEMU YA E (Alama 20 )**

**FASIHI SIMULIZI**

**5. a) Soga-mazungumzo ya kupitisha wakati.(alama 2)**

**b) -Hugawanywa katika beti/stanza.**

**-Huimbwa kutegemea mazingira.**

**-Hutolewa wakati maalum/mahali maalum.**

**-Huimbwa zikiandamana na uchezaji wa ngoma. (zozote 4x1**

**c) Maigizo ni hali ya kuiga matendo,tabia za watu au viumbe. (1x2)**

**d) -Hutolewa mbele ya hadhira.**

**-Uigizaji huhitahi uwanja maalum.**

**-Hufungamana na shughuli za jamii nf. Sherehe za mviga,utambaji hadithi n.k.**

**-Lazima kuwe na tendo la kuigizwa.**

**-Waigizaji huvaa maleba.**

**-Maigizo huiga hali ya maisha ya jamii.**

**-Yaweza kuambatana na ngoma pamoja na uimbaji. (zozote 3x2)**

**e)**

**-Kuongeza msamiati katika lugha.**

**-Kupamba lugha.**

**-Kuficha lugha chafu.**

**-Kurahisisha mawasiliano na kufanya wanakundi wajihisi kuwa pamoja.**

**-Kujitambulisha kwa watu na kunndi Fulani. (3x1=3) f)**

**-Huambatana na utamaduni.**

**-Hongozwa na watu maalum.**

**-Hufanya mahali maalum k.v mwituni,kando ya mto n.k.**

**-Hufanywa kwa utaratibu maalum.**

**-Kuna kula kiapo na matambiko kutolewa.**

**-Huambatana na ulumbi/mawaidha.**

**-Sadaka hutolewa (zozote 3x1=3)**